

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

621


KISWAHILI

Muda: Saa 3

Mwaka: 2020

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenyе jumla ya maswali **kumi sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** kwenye chumba mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Tofautisha fasihi simulizi na fasihi andishi katika vipengele yifuatavyo:

(a) Umri (b) Uwasilishaji
(c) Umiliki (d) Hadhira

2. Bainisha sifa nne muhimu ambazo kitabu cha ziada kinapaswa kuwa nazo.

3. "Msomaji mahiri anatakiwa kuwa na sifa kadhaa katika usomaji." Fafanua sifa nne.

4. Eleza kwa kifupi hasara nne za kutumia mbinu ya Masimulizi katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji kwa shule za msingi.

5. Kwa kutumia sentensi zifuatazo andika aina za maneno yaliyopigiwa mstarí:

(a) Mtoto mdogo amenunua kiatu kizuri.
(b) Mama alimwambia Alfred. "Siku zote kaa mbali na mwendawazimu."
(c) Lo! Kizuri kimeshanunuliwa.
(d) Juma anampenda mchezaji yule.
(e) Uvivu wake ulimponza hadi akafukuzwa kazi.
(f) Mwalimu aliwahabarisha wanafunzi kuhusu kufunga shule kwa mwezi mmoja.
(g) Dereva alimtoza abiria nauli kubwa.
(h) Asalale! Nimesahau kumtumia mama zawadi ya sikukuu.

6. Fafanua kwa kifupi kazi nne za mwanafunzi wakati mwalimu anawasilisha maarifa mapya katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

7. Taja mambo manne ya kuzingatia ili kupata ujumbe katika habari inayosikilizwa au inayosomwa.

8. Eleza kwa kifupi tofauti mbili baina ya zana za kufundishia na zana za kujifunzia.

9. Onesha sifa nne za mashairi ya jadi au kimapokeo.

10. Eleza kwa ufupi maana ya maneno yafuatayo:

(a) Kiimbo (b) Shadda
(c) Silabi (d) Mshangao

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. Kwa kutoa mfano kwa kila kipengele, onesha namna ambavyo methali zisipotumika vizuri zinaweza kuleta madhara katika jamii.

(a) Afya (b) Uchumi
(c) Malezi (d) Masuala ya haki
(e) Ushirikishwajii

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali mawili (2) kutoka sehemu hii

12. Wewe ni mwalimu katika Shule ya Msingi Mtinikwetu iliyopo Wilaya ya Nachingwea. Mwandikie barua Afisa elimu wako ukimtaarifu upungufu wa vitabu vya kiada vya somo la Kiswahili.
13. Kwa kutumia mifano, ainisha aina tano za kauli ya utendaji katika lugha ya Kiswahili.

SEHEMU C (Alama 30)
Jibu maswali **mawili** (2) kutoka sehemu hii.

14. Fafanua aina sita za maswali yanayotumika kupima wanafunzi wa shule za msingi, kisha toa mfano kwa kila aina.
15. (a) Shajara la somo ni nini?
(b) Fafanua vipengele vifuatavyo vya shajara la somo la Kiswahili.
(i) Dhana/ujuzi uliofundishwa
(ii) Maoni ya Mkuu wa Idara
(iii) Taarifa za jumla/awali
(iv) Tarehe ya kuanza na kumaliza
16. Eleza hatua sita za kufuata katika kufundisha somo la ufupisho kwa wanafunzi wa Darasa la Saba.